**KENYATTA UNIVERSITY**

**UNIVERSITY EXAMINATIONS 2014/2015**

**INSTITUTIONAL BASED PROGRAMME (IBP) (APRIL 2015 SESSION)**

**EXAMINATION FOR THE DEGREE OF MASTER OF ARTS**

# AKS 815: CONTEMPORARY KISWAHILI LITERATURE

---

**DATE: THURSDAY 27TH AUGUST 2015 TIME: 2.00 P.M. – 5.00 P.M.**

---

**MAAGIZO:** Jibu Maswali Manne. Swali la Kwanza ni la lazima

1. Huku ukitoa mifano inayofaa, fafanua majukumu yanayosawiriwa katika fasihi ya kisasa ya Kiswahili.

2. Mgogoro wa ushairi wa Kiswahili ulioshuhudiwa katika miaka ya 1960 hadi 1980 ni dhihirisho la ustawi wa ushairi wa Kiswahili kama taaluma. Jadili.

3. Tumia mitazamo mbalimbali ya nadharia ya kiutanzi kuainisha mashairi yanayopatikana katika diwani ya Kichomi (E. kezilahabi), Chembe cha Moyo (A. Mazrui) na Sauti ya Dhiki *(A. Abdalla).*

4. Kwa kurejelea riwaya moja ya Ben Mtobwa au M.S. Abdulla na ya J.S. Simbamwene, tathmini dhima ya Sadf[illegible]a taharuki katika usanii wa masimulizi ya kipelelezi.

5. Ainisha na ujadili mihimili ya uhalisiajabu na uonyeshe jinsi inavyojidhihirisha katika kazi mbili zozote za fasihi zilizochapishwa baina ya 2000 – 2014.

6. Jadili maana mbalimbali za dhana ya itikadi huku ukionyesha jinsi zinavyoathiri maudhui ya mwandishi kwa kurejelea kazi za sanaa maalumu.

7. Linganisha na ulinganue ukoloni na ukoloni mambo-leo kwa kurejelea Kinjeketile (E. Hussein) na Kilio cha Haki (A. Mazrui).

---

**INVOLVEMENT IN ANY EXAMINATION IRREGULARITY SHALL LEAD TO DISCONTINUATION**